

## Utambulisho

**Kanisa la Mennonite la Mashariki ya Kanada ni jumuiya changamano**

**Kubadilishwa na upendo wa Mungu**

**Kuongozwa na tumaini tunalopata kwa Yesu**

**Mwito wa kuchukua hatua kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.**

*Tunaamini kwamba Mungu analiita Kanisa la Mennonite la Kanada ya Mashariki kuwa kanisa la Mennonite la Anabaptisti; mshirika aliyefanya maagano katika Kanisa la Mennonite la Kanada na Kongamano la Kimataifa la Mennonite. Huu ni mwendelezo wa desturi ya kihistoria ambayo inasitisiza: Yesu ndiye kitovu cha imani yetu; jumuiya ni kitovu cha maisha yetu; na upatanisho ndio kitovu cha kazi yetu. Kama jumuiya ya makusanyiko, tunatafuta kujunga na utume wa Mungu ulimwenguni, tukiwatia moyo wote kuitikia zawadi ya Mungu ya upendo iliyo funuliwa katika Yesu, kama inavyofafanuliwa katika maandiko.*

## Kusudi

Tunakusanyika kama kanisa la kikanda ili:

- **Kutia nguvu makusanyiko** katika ibada, ufuasi na utume
- **Kuwahimiza viongozi kuhusu tumaini**, maono na mageuzi
- **Kuhifadhi utumishi wa Mungu wa upatanisho** kwa viumbi vyote

## Maadili

**Upendwa** - Watu wote mbele ya Mungu ni sawa na wana hadhi, wameumbwa kwa mfano wa Mungu.

**Uroho** - Ibada na maombi hutuweka katika upendo wa Mungu na kutuunganisha na harakati za Roho.

**Mageuzi** - Tunatamani kuona kile ambacho Mungu anafanya katika maisha yetu na katika ulimwengu. Tunakubali mabadiliko.

**Jumuiya** – Tunakua, tunajifunza na kutumikia vyema katika uhusiano na wengine, tukimsikiliza Mungu pamoja.

**Ukarimu** – Kila mtu anakaribishwa kwenye meza ya neema ya Mungu.

**Amani na haki** – Tunaishi katika Amani ya Mungu kwa viumbi vyote.

Utambulisho, kusudi na maadili yetu hutuelekeza katika maono tunayoshikilia kote nchini kama Kanisa la Mennonite la Kanada:

***Mungu anatuita tuwe wafuasi wa Yesu Kristo na, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ili tukue kama jumuiya za neema, furaha na amani ili uponyaji wa Mungu na tumaini lake litiririke kupitia kwetu kwenda ulimwenguni.***

## Mambo muhimu katika 2022-2027

- **Kushamiri katika Mabadiliko:** Kukuza utamaduni wa kujifunza, uvumbuzi na kubadilika ili kuliwezesha kanisa kushamiri katika mabadiliko. Hii inajumuisha kuchunguza hali mpya za kumfuata Yesu na kuwa kanisa pamoja.
- **Kukuza Viongozi:** Kuimarisha uongozi na kujenga imani, kuwatayarisha watu binafsi kufuata miito yao ya upandaji kanisa, utumishi wa kichungaji na uongozi wa walei.
- **Ufuasi wa vizazi:** Kushirikiana na makusanyiko na washirika wa utumishi katika kuendeleza ufuasi wa vizazi na malezi ya imani, na kuwashirikisha vijana na vijana wa makamo katika fursa za maendeleo ya uongozi.
- **Kukumbatia Utofauti:** Kualika na kutoa changamoto kwa kanisa ili kuchunguza aina na utajiri wa watu wa Mungu. Hili litahitaji mabadiliko ya mioyo, nia, sera na miundo yetu tunapoishi kulingana na wito wetu wa kuwa kanisa tofauti, jumuishi na la kitamaduni.
- **Kutafuta Amani na Haki:** Kusaidia na kufadhili makusanyiko ili kuhusisha masuala ya amani na haki, yanayojikita katika theolojia ya Anabaptist-Mennonite. Uhusiano wa Wenyeji-Walowezi, hatua za hali ya hewa, kujenga uwezo kati ya tamaduni na kutengua ubaguzi wa rangi ndiyo masuala yanayozingatiwa wakati huu.